# MAJANGA NA JUKUMU LA JAMII

الكوارث ومسؤولية المجتمع

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hasan Musa as-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul-Karim Juma Nkusui

ترجمة

# الكوارث ومسؤولية المجتمع

تأ ليف
الشيخ حسن بن موسى الصفار

من اللغة العربية الى اللغة السواحلية

**© Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
Al-Itrah Foundation

**ISBN No:** 978 - 9987 – 17 – 073 – 9

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hasan Musa as-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul-Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba na Alhaji R. S. K. Shemahimbo

**Kimepitiwa na:**
Mubarak A. Tila

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Octoba, 2014
**Nakala:** 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** w.w.w.alitrah.info

# Majanga na Jukumu la Jamii
# Mazungumzo Katika Siku ya Arobaini ya Tukio Chungu la Msiba

# YALIYOMO


Neno la Mchapishaji ........................................................................ 1

Utangulizi.......................................................................................... 3

Majanga na Jukumu la Jamii............................................................ 4

Mtihani Humwendeleza mtu na Ummah .......................................... 5

Nchi na Majanga ............................................................................. 10

Ajali ya Moto Ulioteketeza Qadihi ................................................. 10

Mafunzo Kutokana na Janga Hili .................................................... 11

Mshikamano waTaifa...................................................................... 12

Mshikamano wa Kijamii na Asasi za Kiraia.................................. 13

Nyendo Zinazohitaji Kurekebishwa ............................................... 15

Mimi na Wewe ni Nukta ya Kwanza ............................................. 16

Amani na Usalama........................................................................... 17

Funzo Katika Kukabiliana na Majanga........................................... 18

بسم الله الرحمن الرحيم

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha lugha ya Kiarabu kwa jina la, *al-Kawarithu wa Mas'uliyyata 'l-Mujtama',* kilichoandikwa na Sheikh Hasan Musa as-Saffar. Sisi tumekiita, *Majanga na Jukumu la Jamii.*

Mwandishi wa kitabu hiki anazungumzia matukio ya majanga mbalimbali kama vile mitetemeko ya ardhi, mafuriko, vimbunga na ajali. Kwa kawaida, wanadamu huyaona majanga haya kama balaa au shari fulani iliyowapata. Kwa hivyo, kwao inakuwa ni msiba mkubwa.

Hata hivyo, mwandishi, Sheikh wetu huyu anatukumbusha kwamba ingawa sisi tutayatafsiri majanga kama balaa na msiba kwetu, lakini majanga mengine ni heri, kama utakavyosoma katika kitabu hiki na mengine ni adhabu. Kwa hivyo, inatakikana tafakari na subira ya hali ya juu sana yanapotokea majanga. Uislamu umeweka kanuni ya maombi yanapotokea majanga ya aina hii (yaani, swala ya majanga). Maombi haya kwanza ni kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa Utukufu Wake; na pili, kumuomba atukinge na atufanyie wepesi kutokana na majanga hayo.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Kutoka na ukweli huu, taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumini

yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Abdul-Karim Juma Nkusui kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukitarjumi kitabu hiki kwa Kiswahili kutoka lugha ya asili ya Kiarabu. Aidha tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

**Mchapishaji:**
**Al-Itrah Foundation**

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

***Kwa jina la Mwenyezi Mungu***
***Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu***

Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe, Swala na salamu zimwendee Nabii wetu Muhammad na kizazi chake kitwaharifu na Masahaba wake wema.

Jamii katika kila hatua ya mwendo wake inahitaji maarifa sahihi, yanayoionyesha uhalisia wake na yanayofungua mbele yake upeo wa matumaini na maendeleo na kuisaidia katika kukabiliana na changamoto na vikwazo. Na ili maarifa yatimize jukumu lake kwa wanajamii na yafanyie kazi nguvu zake na kunoa azma yake kuelekea kwenye maendeleo, ni lazima maarifa hayo yawe na sifa zifuatazo:

- Yawe ni ya asili yanayotokana na maadili sahihi ya jamii ya kidini.
- Yawe ya kisasa yanayoendana na mabadiliko ya maisha na mabadiliko ya kifikra.
- Kutokana na maarifa hayo, upatikane mkakati unaokidhi haja ya jamii na mahitaji yake.

Na yamiliki lugha ya kuzungumza na watu wa makundi yote na wa viwango mbalimbali, bila kuzama kwenye nadharia tupu na istilahi za ubobezi zilizoenea katika hotuba za makhatibu, kwa sababu kuzungumza na watu wa kawaida kunahitaji uwezo mkubwa

wa uwazi, na wa kutatua mambo halisia yaliyopo. Hivyo kundi la jamii lenye maarifa kati ya maulamaa, wanafikra na wanafasihi wao ndio upande wenye jukumu linalokusudiwa la kuzalisha na kuleta maarifa haya yanayohitajika.

Na kwa sababu hii na katika upande huu, Mwadhama Sheikh Hasan as-Safar – Mwenyezi Mungu amhifadhi – amekuwa akitoa maarifa haya ya kukuza uwelewa kupitia uandishi, hotuba na hadhira kubwa ya kijamii. Na silsila hii ya vitabu ni uhariri wa baadhi ya mihadhara ambayo aliitoa katika minasaba mbalimbali, na hivyo kitengo cha utamaduni katika ofisi ya Sheikh kimeiandika na kuiandaa kwa ajili ya kuchapishwa hali wakitaraji kwamba itachangia katika kusambaza uelewa na kueneza fikra zenye kujenga na kustawisha maarifa katika jamii. Na wanataraji kuwa Sheikh atapata malipo na tawfiki ya ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kutoa na Mmiliki wa tawfiki.

## MAJANGA NA JUKUMU LA JAMII[1]

Mwanadamu katika maisha anakabiliwa na matarajio na mabadiliko, kama ambavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu anammiminia neema Zake na kheri Zake, hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anaweza pia kumpa mtihani na balaa kwa kumjaribu kwa matatizo na mishkeli ya aina mbalimbali. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ وَنَبْلُوكُمْ بِالشَّرِّ وَالْخَيْرِ فِتْنَةً وَإِلَيْنَا تُرْجَعُونَ

[1] Muhadhara uliotolewa siku ya Ijumaa tarehe 30/5/ 1420 sawa na 10/9/1999 katika mnasaba wa Arobaini ya siku ya tukio baya na chungu la Karbala.

**"Kila nafsi itaonja mauti. Na tutawajaribu kwa mtihani wa shari na kheri, na Kwetu mtarejeshwa." (Sura Anbiyai: 35)**.

Aya hii tukufu inazingatia kwamba chochote kinachomkabili mwanadamu katika maisha yake hakika kinatokana na kazi ya mtihani au balaa kwa aina zake mbili: Kheri na Shari. "Na tutawajaribu," yaani tutawatahini. (kwa mtihani wa shari na kheri). Hakika kile ambacho mwanadamu anaitakidi kuwa ni shari au kheri sio shari wala kheri kwa maana halisi, bali mwanadamu ndiye anayeitakidi hivyo. Mwenyezi Mtukufu anakutahini kwa yale ambayo wewe unayazingatia kuwa ni shari, lakini je, kweli mambo hayo ni shari au sio shari, huu ni utafiti mwingine.

Maradhi – kwa mfano – mwanadamu anayazingatia kuwa ni shari, lakini kwa uhakika sivyo hivyo, kwa maana ya jumla, bali ni shari kwa mazingatio tu. Ni maradhi mangapi yameleta kinga kwa mwenye maradhi hayo, na ni maradhi mangapi madogo yamepelekea kugundulika maradhi hatari katika mwili wa mwenye maradhi. Na lau kama si vipimo vilivyofanywa kwa ajili ya kutibu ugonjwa mdogo, yasingegundulika maradhi hatari na kujulikana. Hakika kila yanayotokea kwenu ni mtihani na ni kujaribiwa.

## Mtihani Humwendeleza Mtu na Ummah:

Hakika mtihani unaweza kutazamwa katika maana mbili: Mtihani wa duniani, na mtihani wa Akhera. Ama mtihani wa duniani hakika unatarajiwa kuleta maendeleo katika uwezo wa mwanadamu katika kukabiliana na changamoto za maisha, na hiyo ni wakati mwanadamu anapohisi kuwa anakabiliana na changamoto ambayo ni lazima kwake kuishinda, vinginevyo namna gani mwanadamu ameweza kubadilisha njia za maisha na mbinu za maisha na aina ya makazi na njia za usafiri n.k, kama asingekuta

nafsi yake inahitaji kushinda changamoto za mazingira ambayo yanamkabili.

Hakika ugunduzi na uvumbuzi umepatikana kwa kukabiliana na changamoto na mahitaji, kwa mfano kuendelea kwa elimu ya tiba, na hususan maendeleo ya haraka ya utafiti wa misingi ya kurithi tunayoyashuhudia sasa yasingetokea kama mwanadamu asingekabiliana na matatizo ya maradhi hatari na kuugua, kama ilivyosemwa: Shida ni mama wa uvumbuzi. Kila mwanadamu anapopatwa na hatari au balaa anatafakari kwa makini namna ya kuvuka hatari hiyo na kuepukana na balaa hiyo.

Hakika sisi tunadhani kwamba Mwenyezi Mungu ameumba maisha kwa matatizo yake na ugumu wake ili amtahini huyu mwanadamu je, ataibua nguvu zake na atatumia vipaji vyake kwa ajili ya kukabiliana navyo au hapana? Hapa unakuta kuna aina mbili za watu katika kukabiliana na ukweli huu:

**Aina ya kwanza:** Yupo ambaye hakabiliani ili kutatua matatizo yake isipokuwa pale tatizo linapombana sana, na kumuweka katika hali mbaya na shida kiasi cha kutokuweza kuvumilia, wakati huo anatafakari katika kutatua tatizo.

**Aina ya pili:** Ni yule ambaye anatafakari katika kutatua tatizo kabla ya kutokea au kuibuka, au tuseme yule ambaye anatafakari mfumo wa kinga na sio tiba na anaitakidi kwamba diriham ya kinga ni bora kuliko mamilioni ya tiba (kinga ni bora kuliko tiba kama walivyosema wahenga). Hakika dhana ya uwepo wa tatizo – kabla ya kutokea – ndio pekee ambayo inayomsukuma kutafakari katika mipango yake. Na kwa maana nyingine tunaweza kueleza kuwa mtihani ni kwa ajili ya kupanga hatima ya mwanadamu Akhera, na hiyo ni kwamba balaa hii inavumbua asili ya msingi na itikadi ambayo anaibeba mwanadamu ndani yake mbele ya Muumba, bali inavum-

bua uhalisia safi na kukinai kwake ambako anajipamba nako mbele ya mitihani hii. Je anabeba subira na shukrani au ukafiri na ukanushaji? Je ana chochote kati ya ridhaa na kujisalimisha au amesheheni hasira na chuki? Je anategemeza mambo yake yote kwa Mwenyezi Mungu au anamtafuta hata  shetani ili amkomboe? Na je, yakini yake kwa rehema ya Mwenyezi Mungu na hekima yake vinamfanya awe na matumaini na kuridhia au ni kinyume chake?

Hakika mwanadamu hatodumu katika maisha haya lakini hakika atadumu katika maisha ya Akhera:

وَمَا هَٰذِهِ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا لَهْوٌ وَلَعِبٌ وَإِنَّ الدَّارَ الْآخِرَةَ لَهِيَ الْحَيَوَانُ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ

**“Na maisha haya ya dunia si chochote ila ni upuuzi na mchezo. Na nyumba ya akhera ndiyo maisha hasa, lau wangelikuwa wanajua.” (Sura Ankabut: 64)**.

Na ili upate kudumu katika pepo yenye neema ni lazima kukabiliana na mtihani wa kheri na shari kwa kufaulu. Na inaweza kukusaidia ewe mwanadamu katika kukabiliana na mbinyo wa maisha ile kujua kwako kwamba mbinyo wake ni wa muda tu na hautoendelea kwa muda mrefu halafu mambo yote yatarejea kwa Mwenyezi Mungu, yaani hakika huo ni mtihani **“Na Kwetu mtarejeshwa.” (Sura Anbiyai: 35)**.

## Vipi Tutakabiliana na Majanga?

Hakika matatizo na balaa ambazo zinawasibu watu ziko aina nyingi:

1. Miongoni mwayo ni yale yanayosababishwa na mazingira kulingana na muundo na muweko wake.

2. Na miongoni mwayo ni yale anayoyasababisha mtumiaji mwenyewe wa mazingira na mwenye kuyaendeleza.

Na katika aina ya kwanza ya majanga hayo ya kimazingira, ambayo yanatokea baina ya wakati mmoja na mwingine ni kama vile matetemeko, volkano, mafuriko, maporomoko ya udongo au barafu, vimbunga n.k.

Na tetemeko ambalo lilipiga mji wa Azumit na Istanbul Uturuki ni moja kati ya majanga hayo, waliofariki katika waathirika wa tetemeko ni zaidi ya watu 14,000, ama majeruhi ni zaidi ya 40,000 na ama hasara ya mali inatosha kujua kwamba kiasi kinachohitajika ili kufidia hasara iliyotokana na uharibifu na kukwamisha harakati za kiuchumi inazidi dola bilioni 25.

Kama ambavyo watu binafsi wanatofautiana katika kukabiliana na mtihani yao pia ndivyo mataifa yanavyotofautiana katika kukabiliana na mitihani yao. Na vivyo hivyo tunakuta katika tetemeko hili uhalisi mwingine nao ni kufeli katika kukabiliana na mtihani kabla ya kutokea kwake na baada ya kutokea kwake.

Pamoja na kwamba Uturuki iko katika mstari wa matetemeko isipokuwa ni kwamba, si serikali wala wananchi wa Uturuki waliokuwa wamejiandaa kukabiliana na janga, na kinachochekesha na kuliza ni kwamba serikali ya Uturuki ilidhihirisha ugomvi wake na harakati za Kiislamu hadi kwenye kilele cha juu cha mzozo na fazaa ambayo iliwaenea watu baada ya tetemeko. Serikali ilizuia taasisi za wananchi na za kijamii za Kiislamu kusaidia kupunguza athari za tetemeko kwa sababu serikali haikutaka taasisi hizi kupata umaarufu na uungwaji mkono wa wananchi wa

kimaanawi na kuongeza umaarufu wake mkubwa, bali ilitaka kuwaengua na kuwakomoa hata katika mfano wa janga hili ingawa mwananchi wa Uturuki ambaye inatarajiwa kuwa pande mbili zingeshindana katika kumtumikia, katika hali hii amekuwa ndio muhanga.

Ama aina ya pili ya majanga ni yale ambayo yanasababishwa na mtumiaji wa mazingira, na ambayo inawezekana kuyaita ajali za utengenezaji. Mfano ajali za magari, treni, ndege, kuzama na ajali za moto na kutokea milipuko katika viwanda vya silaha na kuvuja mafuta katika meli za usafirishaji baharini na mengineyo mengi ambayo yanasababisha kutokea kasoro ambazo zinapelekea kutokea majanga hayo na kufariki waathirika na kuharibu mazingira na kusambaa maradhi, kama ilivyotokea katika ajali ya kiwanda cha dawa za kuulia wadudu katika mji wa (Bahubal) India tarehe 17 Desemba 1984, ilipotokea kuvuja gesi hatari ya (*Izosyernet alymetal*) kutokana na kosa la kiufundi kwa sababu ya usimamizi mbaya. Na inazingatiwa kuwa kiwanda hiki ni cha pili katika ulimwengu katika kuzalisha gesi hii yenye sumu kali, nayo ni gesi ya kimiminika kisicho na rangi chenye kulipuka haraka. Na maelefu walipoteza macho yao katika sehemu ya Bahubal ambayo idadi ya wakazi wake inafikia watu 672,000, na walifariki zaidi ya watu 2500 na zaidi ya watu 3000 walipatwa na maradhi ya hatari. Na vilevile janga la Tchernobil katika kiwanda cha nyuklia cha Soviet.

**Nchi na Majanga:**

Kwa huruma za Mwenyezi Mungu Mtukufu, hakika ameepusha nchi yetu (Saudi Arabia) na ajali na majanga mengi, na huenda miongoni mwa majanga yaliyoisibu nchi ni:

**Kwanza:** Janga la kimazingira, nalo ni kimbunga kikubwa ambacho kilitokea usiku wa Ijumaa tarehe 13/3/1344, yaani miaka 76 kabla ya sasa, na kiliendelea kwa muda wa nusu saa takriban, na kilisababisha kuanguka kwa maelfu ya mitende, miti, vibanda kubomoka na baadhi ya majumba kuporomoka. Na lililo baya zaidi kuliko hayo ni kuzama kwa makumi ya waogeleaji na mabaharia ambao walikuwa wanafanya kazi ya uzamiaji na ubaharia, na mwaka huo ambao lilitokea tukio hilo ukaitwa Mwaka wa Twaba'ah, na ukawa ni historia inayoandikwa.

## Ajali ya Moto Ulioteketeza Qadihi

Ama janga la pili ambalo liliikumba nchi ni katika aina ya pili ya majanga, nalo ni ajali ya moto mkubwa na ambao uliiteketeza Qadih tarehe 16/4/1420, na huwenda ndio tukio baya zaidi na chungu zaidi lililoipata nchi yetu, idadi ya waliopoteza maisha imefikia watu 70 hadi hivi sasa, ama majeruhi ni zaidi ya watu 154, baina yao watu 80 majeraha yao ni mabaya mno.

Ikiwa waliozama katika mwaka wa Twaba'ah walikuwa ni kati ya watu wenye nguvu wenye kujiandaa kwa ajili ya kupiga vita majanga na hatari, hakika waliofariki katika ajali ya moto ya Qadihi hawakuwa isipokuwa wanawake dhaifu, watoto wadogo na wasichana walio katika umri wa ujana.

Na mwanadamu katika msiba mkubwa kama huu hana la kufanya isipokuwa ni kutegemeza jambo hilo kwa Mwenyezi Mungu na kukariri kauli Yake (swt): "Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na hakika sote tutarejea Kwake."

**Mafunzo Kutokana na Janga Hili:**

Pamoja na tukio la msiba na ukubwa wa janga, haipasi sisi kuamiliana na hali iliyotokea kwa kukomea tu katika mipaka ya upole na huruma, bali ni wajibu wetu kuchukua funzo na mazingatio na kuamiliana na athari za tukio hili na matokeo yake kwa namna ambayo itaongeza kitu katika hazina yetu ya malezi na imani kwa kunufaika katika nyanja na pande mbalimbali kutokana na msiba huu.

Tukio hili limedhihirisha nukta nyingi zenye nguvu, kama ambavyo limefichua baadhi ya nukta za udhaifu, hivyo ni juu yetu kuzidhihirisha nukta hizi ili tujue ni sehemu zipi tuna nguvu na ni sehemu zipi tuna madhaifu, ili tuimarishe nukta zetu zenye nguvu na tuziendeleze, na tuondoe nukta za udhaifu na kufuta athari zake.

## HURUMA YA KIIMANI HAITAMBUI MIPAKA

Hakika somo la kwanza ambalo limefichuliwa na tukio hili ni kwamba kuna hali ya huruma ya kiimani ambayo inavuka mipaka yote ya migawanyiko ya kisiasa na kijiografia. Janga hili lilitokea katika kijiji kimoja katika nchi lakini waumini kutoka kila sehemu miongoni mwa wale waliofikiwa na habari ya tukio hili walishughulika na waliamiliana na waathirika kwa huruma kana kwamba msiba umewatia uchungu moja kwa moja. Wakawa wanafuatilia habari za tukio muda baada ya muda, na ujumbe wa rambimbi ukatumwa kwa watu wa Qadihi na maulamaa wa eneo hili kutoka kwa maulamaa wakubwa na Marjaa watukufu, kutoka ndani na nje, kwa kuwapa taazia kwa msiba na kuelezea masikitiko yao na huzuni yao kwa tukio lenye kutia machungu. Na vilevile wakapokea ujumbe wa rambirambi na ujumbe wa kuwapa pole na kuwaliwaza kutoka kwa waumini wengine wa sehemu mbalimbali za ulimwengu. Kama ambavyo pia

zilifanywa majilisi za maombolezo katika sehemu mbalimbali ulimwenguni, na wakaja wageni kutembelea nchi kwa ajili ya kutoa rambirambi na pole kutoka Baharain, Kuwait, na sehemu nyinginezo.

Kipi kilichowafanya hawa watu wa Syria, Iran, Lebanon, Pakistan, India na kila sehemu katika ulimwengu wajihusishe na msiba huu? Yapi yaliyowafanya waamiliane kwa huruma pamoja na sisi katika tukio hili? Je, ni imani ndio inayounganisha hisia za wote, au je ni zile hisia zao kwamba hawa ni waumini wanaofanana nao katika itikadi na misingi? Yote hayo yalikuwa ni dalili kubwa ya huruma ya kiimani na hisia moja, kama ilivyopokelewa katika hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu rehema na amani zimshukie yeye na kizazi chake na masahaba wake wema, kuwa: “Mfano wa Waumini katika kupendana kwao na kuhurumiana kwao na kuamiliana kwao ni mfano wa kiwiliwili kimoja, kinapoumwa kiungo kimoja katika mwili, basi mwili wote unaumwa na kukesha na homa.”[2]

**Mshikamano wa Taifa:**

Na hili tukio chungu la kitaifa limedhihirisha mshikamano mzuri wa kitaifa, viongozi wa serikali waliongozwa na makamu, Amir Abdillahi bin Abdul- Aziz (hiyo ilikuwa ni kabla ya hajawa mfalme) ambaye alijitolea kuwapa pole wananchi wa sehemu (husika) kwa kutoa ujumbe mzuri uliojaa upendo, upole na huruma, na akawa kama tabibu ambaye anatibu majeraha ya majeruhi waliojeruhiwa, kama ambavyo aliamuru kuchukuliwa hatua za haraka za kutibu majeruhi, kisha akahitimisha upole wote huo na ukarimu kwa uamuzi wa kuanzisha ukumbi kwa ajili ya sherehe za furaha kwa watu wa Qadih, chini ya usimamizi wa jumuiya yao ya kheri, Mwenyezi Mungu amlipe kheri na amfanye kuwa ni ukumbusho kwa wananchi na nchi.

[2] Al-Hindiy: al-Mutaqiy bin Hasaam Diyn katika *Kanzul-Umaal fiy Sunanil- Aquwwaal wal-af'aal*, chapa ya tano 1985 Muasastu risaala–Beirut Juz. 1, uk. 149 hadith namba 737

Na wanachi katika kiwango cha kitaifa pamoja na kutofautiana sehemu zao, makabila yao na madhehebu yao lakini walionyesha mshikamano wao mkubwa, na walitoa msaada wao wa kimali na kimaanawi katika kijiji kilichopatwa na tatizo. Na waandishi, wanafasihi na wanahabari wa Kisaudia toka sehemu mbalimbali na wenye mitazamo mbalimbali walielezea moyo huu wa umoja wa kitaifa, katika maandishi yao, mashairi yao na uhakiki wao wa magazeti na ufuatiliaji wao wa habari.

Mshikamano huu mkubwa wa kitaifa ni hazina ya kimaanawi muhimu ambayo ni wajibu kuihifadhi, kuikuza na kuiendeleza kwa kuifanya kuwa ni hali ya mawasiliano ya kudumu yanayovuka mipaka ya jiografia, ukabila na madhehebu.

**Mshikamano wa Kijamii na Asasi za Kiraia:**

Na kupitia tukio hili chungu kimedhihirika kiwango cha juu cha mshikamano wa kijamii, ambapo walianza watu wa Qadih kwanza kuamiliana na tukio hili kana kwamba ni familia moja, na kijiji kwa familia zake mbalimbali na tabaka zake mbalimbali za kimakazi kikawa ni nyumba moja, na mshikamano wao katika kushughulikia matokeo ya tukio na uelewa wao katika kuamiliana na mapungufu na athari zake ulikuwa katika kiwango kizuri cha mshikamano na utekelezaji. Jaribio la kuwanusuru waliojeruhiwa na kuwapeleka hospitalini na usindikizaji mkubwa waliofanyiwa wale walioaga maisha, na majilisi kubwa za maombolezo ambazo zilifanywa Qadihi, kisha kujitokeza kwa wananchi tangu mwanzo wa tukio na kusaidiana kwao kuanzia Swafuwa hadi Sihata, na kila sehemu kuwa pamoja nao, yote hayo yamedhihirisha daraja ya juu ya mshikamano wa kijamii unaotokana na kina cha imani, mshikamano wa kweli na umoja wa jamii moja.

Na jumuiya ya mambo ya kheri ya *Mudhari*[3] ya Qadih ilikuwa na mchango wa kipekee katika kuendesha mambo, ambapo ilgeuka kuwa kituo chenye sura nzuri chenye kuelekewa na watu wa Qadihi, na kitovu ambacho pembezoni mwake kinazungukwa na juhudi, na hapo zinakutana jitihada, na hapo kazi na huduma zinaunganishwa. Jumuiya hii ilisaidia kusimamia wajibu uliotokana na tatizo hili na kusimama pamoja na jumuiya nyingine za mambo ya kheri za nchini, na zikaweka nguvu zake katika kuhudumia waathirika.

Na hii inasisitiza umuhimu wa nafasi ya jumuiya za mambo ya kheri kama vile asasi za kiraia, kwamba zinaweza kufanya jukumu kubwa katika kuhudumia jamii na kukabiliana na matatizo ya maisha na matukio ya majanga. Hapa ni lazima tuelekeze wito wetu kwa kila mwanajamii kwa kuwataka wajiunge kwa wingi zaidi katika jumuiya za mambo ya kheri za kijamii zilizopo katika maeneo yao na wazisaidie kwa mali, mawazo na msaada wa kimaanawi.

Na inasikitisha sana kuona yanajikariri malalamiko ya jumuiya kwa sababu ya watu kutokujishughulisha kwa umakini na uhakika katika uchaguzi wa jumuiya na kukataa kubeba majukumu yake, na kuacha kuzisaidia kwa msaada wa hali na mali. Na kinachosikitisha pia ni baadhi ya jumuiya, vilabu na asasi za mambo ya kheri kugeuka vijiwe vya mazungumzo mabaya na vikao vibaya ambavyo havina umuhimu isipokuwa kutafuta mabaya tu, udhaifu, kasoro na makosa na kuyakuza na kuyaelekeza kwa watu wenye dhamana katika asasi hizi.

Hakika anayetafuta makosa katika asasi hizi na kutafuta kasoro zake ni wajibu wake pia ajue kwamba mazingira ya kazi ya binad-

---

[3] Jumuiya ya Mudhari ya kheri ilianzishwa Qadihi mwaka 1387 Hijiria na ilisajiliwa rasmi katika wizara ya mambo ya jamii kwa namba 9 mwaka 1389 Hijiria

amu yanaambatana na makosa, kwa sababu wanaotekeleza kazi hizo ni binadamu na sio malaika, na hivyo wanakabiliwa na makosa na wao sio maasumina. Na utatuzi wa kosa lolote unapasa uendane na mahali ulipotokea, wakati wake na mazingira yake maalum, hivyo mwenye nia nzuri ya kusahihisha makosa ya asasi hizi atafanya hivyo kupitia muamala mzuri na ushirikiano wa kuhudhuria, kutoa rai na kubeba jukumu na sio kwa kutuhumu na kushabikia. Hakika asasi hizi ni zetu sote, hivyo twende mbio kwa ajili ya kuzihifadhi kwa nguvu zetu zote.

**Nyendo Zinazohitaji Kurekebishwa:**

Ama somo la mwisho ambalo tunaweza kuliashiria ni kwamba ni wajibu wetu kutathmini kwa uhalisia na ushujaa baadhi ya nyendo zetu na vitendo vyetu. Na kwa kuwa mnasaba ambao umetokea nasi tumo katika bahari yake pana, ni mnasaba wa kuoa basi hapa ni lazima tuashirie suala la ukubwa na kupindukia kwa gharama za sherehe za ndoa, kiasi cha kusababisha usumbufu mkubwa wa kimali, taabu na mkanganyiko katika jamii, na kila wakati zinaongezeka ada mpya na mazoea mapya, kiasi cha kufanya kuoa kuwa ni shughuli yenye gharama nyingi na vikwazo vigumu.

Hakika kukodisha mahema kunagharimu kiasi cha mali cha kawaida, na baadhi wameanza kuongeza viti na meza katika mahema. Ama kumbi za sherehe, kwa habari zilizopo ni kwamba zinakodishwa kwa maelfu ya fedha, pungufu au zaidi, kama inavyonukuliwa! Na baadhi wameanza kufanya sherehe za harusi katika hoteli za daraja la kwanza! Hakika kama mambo haya yatageuka na kuwa ada na mazoea ya watu hakika yatasababisha taabu nyingi na mbinyo wa kiuchumi kwa watu na hususan ukizingatia hali ya kiuchumi ya sasa. Hakika tuna Husainiya pana hivyo ni wajibu kutoifanyia ubakhili, na dai la kwamba wake zetu katika minasaba ya

harusi na sherehe, wao na watoto wao wanasababisha matatizo ya kusafisha Husainiya na kuing'arisha kwake, madai haya yanaweza kutatuliwa kupitia makampuni ya usafi na ufuaji mazulia.

Kama ambavyo inapasa kujitolea kuanzisha kumbi za sherehe za kijamii kwa ajili ya manufaa ya wanajamii, kiasi kwamba zitachukua gharama ndogo inayofaa na sio kama kumbi za sherehe za biashara za vitega uchumi, na haya ni mambo ambayo yanapaswa kutekelezwa na kusimamiwa na jumuiya za mambo ya kheri, taasisi za hafla za harusi za pamoja na masanduku ya kuozesha ya kujitolea. Na pia baadhi ya watu wema wajitolee kuanzisha kumbi za sherehe kama wakfu wa kheri, na kufanya hivyo ni katika sehemu ya kheri na wema, kwa sababu katika hayo kuna kuwahudumia watu na kuchangia katika kurahisisha mambo ya ndoa na kulinda familia zetu na watoto wetu kutokana na hatari.

**Mimi na Wewe ni Nukta ya Kwanza:**

Hakika sisi sote tunajua madhaifu na kasoro ambazo jamii yetu inaishi nazo, na tunajua mara nyingi njia ya kuyatatua na kuyamaliza, lakini tatizo ni kwamba baadhi ya tabia za kimakosa zinaota mizizi katika jamii hadi zinakuwa ni ada madhubuti ambayo mtu hawezi kuikiuka na kuikhalifu. Na katika kadhia ya ndoa kuna mengi miongoni mwa mambo haya, kuanzia na tabia ya kuzidisha mahari na gharama za sherehe mbalimbali, kuwa na walima mkubwa kwa ajili ya wanaume na wanawake, pia katika kupamba, mashela ya ghali ambapo mpambe ana shela lake na Bibi harusi ana shela lake, na sio tu Bibi harusi bali na jamaa zake wa karibu na marafiki zake pia.

Na kama ukifanya hesabu ya kubainisha idadi ya watu ambao hawataki mambo haya ambao wanaona uzito wake bali wanatamani

yaondoke haraka, utagundua kwamba wao ni wengi katika jamii, lakini tatizo kila mmoja anakwambia: Hakika fulani alipooa alifanya kadha na kadha na mimi naona aibu kutofanya kama alivyofanya yeye. Vivyo hivyo tunajikuta tunakataa makosa haya kwa kauli na tunayafanya kivitendo na kitabia:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ
كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللَّهِ أَنْ تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ

**"Enyi mlioamini! Kwa nini mnasema msiyoyatenda? Ni chukizo kubwa kwa Mwenyezi Mungu kusema msiyoyatenda."**
**(Surat Swaf: 2– 3)**.

**Amani na Usalama:**

Na upande mwingine wenye kasoro kwetu, unahusu fikra zetu kuhusu usimamiaji wa amani na usalama katika mikusanyiko yetu. Wakati katika jamii zilizoendelea suala la kutafakari katika jambo la amani na usalama ni moja ya masharti ya kufanyika mkusanyiko wowote ule mkubwa, kwetu sisi kutafakari katika jambo hili si suala muhimu, bali baadhi wanazingatia kuwa ni katika aina za usumbufu wenye kuchosha, na kwa hiyo unakuta mikusanyiko yetu katika minasaba yetu ya kijamii au ya kidini inafanyika bila ya kujali jambo hili.

Ni sahihi kwamba mambo yote yako katika uangalizi wa Mwenyezi Mungu, lakini tahadhari na kujihami ni jambo linalotakikana, Mwenyezi Mungu anasema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا خُذُوا حِذْرَكُمْ فَانْفِرُوا ثُبَاتٍ أَوِ انْفِرُوا جَمِيعًا

**"Enyi mlioamini! Chukueni tahadhari yenu! Tokeni vikosi vikosi au tokeni nyote pamoja." (Sura Nisaa: 71)**.

Kwa nini hatufikirii kuweka ufumbuzi wa dharura yoyote itakapotokea? Vipi kama itatokea hitilafu ya umeme? Namna gani kama itatokea ajali ya moto? Je inafaa Msikiti au Husainiya kuwa na mlango mmoja tu wa kuingilia, bila ya kuwepo na vifaa vya kuzima moto? Je kuna maandalizi gani katika maeneo ya umma na maeneo ya huduma?

Hakika wakati idara za serikali zinapowataka baadhi ya watu kutimiza na kuandaa baadhi ya vifaa na masharti fulani, utawakuta wanachukia na wanajaribu kukwepa maandalizi hayo, na wanazingatia kuwa ni vikwazo katika kazi. Hakika dhana hii ni ya makosa, hakika maandalizi ya usalama na vifaa vya usalama ni kitu muhimu na ni dharura na hususan katika sehemu za mkusanyiko.

**Funzo Katika Kukabiliana na Majanga:**

Amesema Amirul-Muuminina Imam Ali bin Abi Twalib (as):

"Katika majanga hujulikana uhalisia wa wanaume."[4]

Ni wazi kwamba mwanadamu anapoishi katika mazingira ya kawaida hakika hali hiyo inaweza kushindwa kufichua utu wake, lakini anapoishi katika hali isiyokuwa ya kawaida – aghilabu – vi-

[4] Al-Amadiy Tamiymiy: Abdul-Wahid katika *Ghurarul-hikam wadurarul- Kalim* mkusanyiko wa maneno ya hekima za Imam Ali (as) chapa ya kwanza1987 Muasasatu al-alamiy ya uchapishaji – Beirut Juz. 2, uk. 53

tendo vyake vya kawaida na ambavyo si vya lengo fulani hutokea kwa wingi zaidi kuliko vitendo ambavyo si vya kawaida na ambavyo hutokana na uwiano wa faida au hasara, kama ilivyo hali katika vitendo ambavyo humtokea wakati wa hali ya kawaida na ya kutulizana. Na miongoni mwa mifano ya hali isiyokuwa ya kawaida, ni ile hali ambayo inapita kwa mwanadamu wakati wa ghadhabu, msiba, shida na anapopatwa na adha na janga, katika hali kama hizi hujitokeza vitendo vyake kwa namna ya bila kupanga, jambo linaloweza kukupa chanzo safi cha kujua utu wake na uhalisia wake.

Anasema Amirul-Muuminina Ali (as): "Lakini Mwenyezi Mungu anawatahini waja Wake kwa aina mbalimbali za matatizo."[5] Kama ambavyo hali hii inafichua uhalisia wa watu, vivyo hivyo inafichua uhalisia wa jamii, na kupitia kitendo cha jamii kuamiliana na hali isiyokuwa ya kawaida unaweza kuiweka jamii katika kundi la jamii zilizoendelea au zisizoendelea. Na katika miaka iliyopita umejitokeza katika asasi za kielimu na za kiidara ubobezi unaoitwa elimu ya kukabiliana na maafa.

Na kwa msingi wa fikra hii tunaweza kuuzingatia msiba ambao uliwapata wananchi jamaa zetu na ndugu zetu wa Qadihi kuwa ni kioo safi kinachoakisi hali ya jamii na kiwango au daraja la kukabiliana na matatizo, na katika mwanga wa tukio hili ni wajibu tujiulize: Namna gani tutaamiliana na matatizo na majanga kama mtu mmoja mmoja na kama jamii?

**Kwanza:** Kujihami na matukio na majanga kabla ya kutokea kwake kwa njia ya kuweka mfumo wa tahadhari na kinga na kufanya maandalizi ya amani na usalama na kujali kuchukua kila njia za kinga na kulinda nafsi, heshima na maslahi.

[5] Ibnu Babawaihi al-Qummiy: As-Suduqu Muhammad bin Ali bin Husain katika *Tauhidi,* Darul-Maarifah ya uchapishaji – Beirut, uk. 369

Hakika kudharau na kupuuza ni jambo linakataliwa kisharia na kiakili. Na muumini kuitakidi kwamba mambo yote yako katika uangalizi wa Mwenyezi Mungu na kujisalimisha katika majaliwa na makadara, haimanishi kupuuzia kinga na tahadhari. Imepokewa kutoka kwa Amirul-Muuminina Ali bin Abi Twalib (as) kwamba aliondoka kutoka kwenye ukuta uliokuwa unakaribia kuanguka, na kwenda kwenye ukuta mwingine, akaambiwa: Ewe Amirul-Muuminina, je unakimbia majaaliwa ya Mwenyezi Mungu? Akasema: "Nakimbia kutoka kwenye majaaliwa ya Mwenyezi Mungu na kwenda kwenye makadara ya Mwenyezi Mungu Mtukufu."[6] Hiyo ni kwa sababu majaaliwa inaamanisha uhakika na yakini, wakati ambapo makadara inamaanisha mwenendo na kanuni.

**Pili:** Maandalizi na utayari wa kukabiliana na dharura. Ndiyo, pamoja na maandalizi yote ya tahadhari isipokuwa ni kwamba majanga yanaweza kutokea, ila kuna tofauti kubwa sana yanapotokea wakati kuna maandalizi na wakati hakuna maandalizi. Hakika baadhi ya watu hawaziandai nafsi zao kwa ajili ya hali ya dharura, wala hawana mbinu wala fikra ya kukabiliana na hali ya dharura katika kiwango cha mtu mmoja mmoja na jamii.

**Tatu:** Inapotokea msiba na janga haifai kukaa na kuangalia tu, kama ambavyo pia kukasirika tu hakuna faida yoyote, ambapo kwa kukasirika huko mwanadamu hukosa uwezo wa kufikiria na kufanya kitendo kinachofaa, bali inapasa kudhibiti nafsi na kujitolea kwa kuchukua hatua za awali za lazima za kutatua dharura husika.

Kati ya visa vinavyosimuliwa ni kwamba, mtu mmoja alikuwa anafuatana na dereva, gari likamgonga mmoja wa wapita njia, wakati dereva anasubiri msaada kutoka kwa aliyeandamana naye, wa kumsogeza aliyegongwa, akakuta yule aliyeandamana

[6] Ibnu Babawaihi al-Qummiy: As-Suduqu Muhammad bin Ali bin Husain katika *Tauhidi* Daarul-Maarifah ya uchapishaji na usambazaji – Beirut, uk. 369

naye amekwishazimia, yeye pia anahitajia msaada wa huduma ya kwanza.

Na imeenea katika fasihi ya kiarabu kile kinachoitwa uharaka, na inakusudiwa uharaka wa maamuzi ya kuchagua utekelezaji na kufanya linalofaa. Na sharia tukufu inaamuru wajibu wa kujitolea kuokoa roho inapokabiliwa na hatari, hata kama hilo litapingana na wajibu mwingine wa kisharia. Kama ikiwa wakati wa Swala ni mfinyu na kukawa na mtu anayeghariki katika maji, basi ni wajibu kuacha Swala na kuwahi kumuokoa.

Na iwapo mtu atajikuta yuko mbele ya mtu anayekaribia kufa, aliye katika hali ya kukata roho, hakika sharia inamwamuru kuchukua hatua zinazofaa katika hali hii, ambapo haipasi kwake kuchukua msimamo wa upole na huruma na kuanza kulia na kuomboleza. Ni makuruhu kufanya hivyo mbele ya anayekata roho, bali ni juu yake kufanya haraka kumwelekeza kibla, kama ambavyo ni mustahabu kumtamkisha shahada mbili na itikadi nyinginezo, na kumsomea baadhi ya dua zilizopokelewa na kumsomea Surat Yasin na Swafaat, na kumfanyia mambo mengine ya mustahabu yaliyotajwa mahala pake. Ni wajibu mwanadamu Mwislamu ajifunze namna ya kuamiliana na dharura kwa umadhubuti na ushujaa na kufanya jukumu ambalo linamlazimu.

**Nne:** Kutoa na kujitolea kwa hali na mali: Hakika kushiriki katika minasaba ya maombolezo na misiba katika tukio la Qadihi, lilikuwa ni jambo lenye kushuhudiwa na lenye kuonekana, isipokuwa hii peke yake haitoshi bali ni wajibu kujitolea na kutoa katika nyanja zote kwa hali na mali. Na kama tukitazama gharama na mahitaji ya kimaada peke yake, tutakuta wasimamizi wa kitengo cha misaada, ambao ni jumuiya ya mambo ya kheri ya Mudhar, ina haja ya kiasi kisichopungua riyali milioni kumi kwa ajili ya kukarabati baadhi ya madhara yaliyosababishwa na tukio hili.

Inapasa tuhakikishe kuwa tuna fungu la malipo na thawabu kwa kutoa katika sekta hii na sekta yoyote yenye thawabu na malipo ambayo inastaki utoaji wetu, si tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yetu na kwa ajili ya wengine kwa kusema:

"Mwenyezi Mungu amezifikia sehemu zake kwa baraka zako" Basi hakika hii ni kati ya sehemu bora zaidi za wema na kutoa. Hivyo ni juu ya wapenda kheri na wenye raghaba ya malipo na thawabu wajitolee kutoa, kila mtu kulingana na uwezo wake, na tuna matumaini makubwa kwamba uwezo wa ndugu zetu wa kutoa ni mkubwa na tunaamini kwamba ushiriki wa wafanyabiashara wetu na matajiri wetu utalingana na kiwango cha tukio.

Ilikuwa inawezekana msiba wa tukio hili kumpata mke wangu au mke wako, dada yangu au dada yako, binti yangu au binti yako, lakini Mwenyezi Mungu amewaepusha baadhi na balaa na amelipeleka kwa wengine, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye mamlaka yote. Lakini ili Mwenyezi Mungu atuepushie balaa inapasa tuwe ni watoaji na wenye kujitolea, kwani imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): "Sadaka inazuia aina sabini za balaa."[7] Na ili Mwenyezi Mungu awaponye wagonjwa wetu na wagonjwa wa waumini inapasa tujikurubishe kwa Mwenyezi Mungu kwa sadaka na kutoa, kama ilivyokuja kutoka kwake (saww): "Toeni sadaka na wagangeni wagonjwa wenu kwa sadaka hakika sadaka inazuia balaa na maradhi, nayo ni yenye kuongeza umri wenu na mema yenu."[8] Na ili Mwenyezi Mungu atuzidishie katika riziki zetu na atulipie madeni yetu basi tujitolee kwa ujumla, na kwa ajili ya tukio hili hususan. Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww):

"Teremsheni riziki kwa kutoa sadaka."[9]

---

[7] Al-Hindiy: Ali al-Mutaqiy bin Hasaam Diyn katika *Kanzul-Umaal,* chapa ya tano 1985 Muasastu Risalah – Beirut, uk. 346 Hadith namba 159882

[8] Rejea iliyotangulia uk. 371 hadith namba 16113

[9] Rejea iliyotangulia uk. 351 hadith namba 16012

Ama katika mambo yanayohusiana na lile tunalotarajia kutoka kwa maulamaa wetu na Marjaa wetu watukufu, hakika sisi tunawaamini Marjaa wetu watukufu, Mwenyezi Mungu awatie nguvu, na kwamba watatoa ushirikiano kwa kutoa na kujitolea kwa kushikamana pamoja na wananchi wetu waliopatwa na msiba, na wala hatudhani wao watajizuia kutoa haki za kisharia kwa ajili ya hilo. Lakini kinachotakiwa kwetu ni mambo mawili:

La kwanza: Kuwaelezea sura halisi ya madhara na hasara, na tuwaweke katika uwelewa wa kina wa uhalisia na undani wa tukio chungu, na tuwaeleze wao kiwango kinachohitajika na dharura ya kupata msaada wa mali na wa kimaanawi, na sisi tunaamini kwamba wao hawatopuuza wala hawatokuwa mabakhili wa kutoa msaada wa kimaada na kiroho.

La pili: Ni wajibu wetu vilevile tuombe idhini ya kutumia haki zote za kisharia au baadhi yake katika upande huu, na hatuna shaka kwamba wao wataguswa sana na jambo hili.

**Tano:** Uwezo wa kuunganisha na kuratibu, kwa sababu tatizo la kwanza linalowakabili watu wanaopatwa na janga, ni kwamba hakika wao wanabaki kwa muda mrefu bila kuamini wala kuelewa yaliyotokea. Wanashikwa na bumbuwazi na mkanganyiko. Hivyo inapasa tangu mwanzo - bali wakati wote - kuunganisha juhudi zetu na kuratibu majukumu, kwa kila upande kuwa na jukumu maalum, na kila mtu awe na jukumu maalum ili kusitokee mgongano katika dauru na majukumu na ili kusitokee mgongano na kuhitalifiana, na ili yeyote asitoe umuhimu kwa upande mmoja kuliko mahitaji yake na kuacha upande mwingine ukiwa ni wenye kusahaulika.

Na uwezo wa kuunganisha na kusaidiana haupatikani ghafla wakati wa tukio lililotokea katika jamii, bali inapasa ukuzwe na uen-

delezwe katika mazingira ya kawaida kwa kuwepo ushirikiano wa kudumu katika mema na uchamungu, katika maisha ya watu ndani ya msikiti, Husainiya, jumuiya kilabu, minasaba mbalimbali na katika nyanja zote za maisha.

**Sita:** Kutumia uwezo na vipaji chini ya nembo ya kipaumbele kwa ajili ya kuokoa na kuweka tofauti zetu pembeni. Haisihi kufanya lengo lolote lile kuwa ni moja ya aina ya vikwazo vitakavyozuia kuwahudumia waliopatwa na masaibu na kuzuia kupunguza madhara ya tukio, yaani tukio lolote lile.

Hakika sisi tunakuta kwamba hata dola zenye kugombana wakati zinapopatwa na misiba na majanga hakika zinaweka kando tofauti zao kwa ajili ya kutoa kipaumbele cha kuokoa. Tumekwishaona namna gani  Ugiriki ilituma kikosi cha uokozi na msaada wa kimaada kwa Uturuki ilipopatwa na tetemeko, na Uturuki ikalipa pale ilipotuma kikosi na msaada kwa walioathiriwa na tetemeko lililoupata mji wa Athiena Ugiriki. Na hakika kama nchi yoyote kati ya hizo mbili ingelikataa mchango na msaada wa uokozi au kukataa kupokea mchango kutoka upande mwingine, hilo lisingekubalika kimataifa.

Kwa sababu kipaumbele wakati wa janga ni kuokoa na kuwatibu majeruhi, na katika janga kubwa hayapatikani hayo isipokuwa kwa kukusanya nguvu ya jamii na vipaji vyote bila kujali tofauti zilizopo. Mwenyezi Mungu awarehemu waliofariki katika tukio hili chungu na awape malipo ya mashahidi, na Mwenyezi Mungu awaneemeshe wagonjwa na waliojeruhiwa kwa kuwapa ponyo wapone haraka, na aziimarishe nyoyo za waliopatwa na msiba kwa kuwapa subira na liwazo. Na Mwenyezi Mungu amlipe kila aliyechangia katika kukabiliana na msiba huu mkubwa na kupunguza athari yake kimaada na kimaanawii, amlipe malipo mema. Na Mwenyezi Mungu ailinde nchi yetu na kila baya, hakika Yeye ni Mwingi mno wa rehema.

## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo  Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo  Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu

43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur’ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur’an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -’n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju’l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju’l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam ‘Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja’a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema

89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102 Hukumu zinazomhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu

135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura

181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam ‘Ali (‘a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja’aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Mjadala wa Kiitikadi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Mwanamke na Sharia
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Mahali na Mali za Umma
220. Nahjul-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
223. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi

224. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
225. Maeneo ya Umma na Mali Zake
226. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
227. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
228. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi

## KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi.

## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique